# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA NAM. 4 YA MWAKA 1986 NA KUTUNGA SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA ZANZIBAR YA MWAKA 2018 AMBAYO INAWEKA UTARATIBU WA UUNDAJI NA UENDESHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Matumizi.

3. Ufafanuzi.

### SEHEMU YA PILI
### UANZISHAJI NA UTAWALA WA IDARA

4. Uanzishaji wa Idara.

5. Kazi za Idara

6. Uteuzi wa Mkurugenzi.

7. Kazi na Mamlaka ya Mkurugenzi.

8. Ofisi ndogo Pemba.

9. Wafanyakazi wa Idara .

### SEHEMU YA TATU
### MUUNDO, UUNDAJI NA KAZI ZA VYAMA VYA USHIRIKA

10. Ngazi za Vyama vya Ushirika.

11. Uundaji wa Chama cha Ushirika cha Msingi.

12. Kazi za Chama cha Ushirika cha Msingi.

13. Uundaji wa Chama cha Ushirika cha Kati.

14. Kazi za Chama cha Ushirika cha Kati.

15. Uundaji wa Chama Kikuu cha Ushirika.

16. Kazi za Chama Kikuu cha Ushirika.

**SEHEMU YA NNE**
**USAJILI WA VYAMA VYA USHIRIKA**

17. Usajili wa Vyama vya Ushirika.

18. Taratibu za kuomba usajili.

19. Athari ya usajili.

20. Kukataa kusajili.

21. Rufaa dhidi ya kukataa kusajili.

22. Kufuta usajili.

23. Rufaa dhidi kufuta usajili.

**SEHEMU YA TANO**
**MUUNDO WA MTAJI, HISA NA MALI ZA CHAMA CHA USHIRIKA**

24. Mtaji wa Chama cha Ushirika.

25. Mfuko wa Akiba wa Chama cha Ushirika.

26. Madhumuni ya Mfuko wa Akiba.

27. Masharti ya kugawa ziada.

28. Mikopo na dhamana iliyoruhusiwa na iliyokatazwa.

29. Uwekezaji wa fedha.

30. Matumizi mabaya ya mali ya Chama cha Ushirika.

## SEHEMU YA SITA
## VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO

31. Matumizi ya Sehemu hii.

32. Madhumuni ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.

33. Mahitaji ya Sheria ndogo.

34. Ukataji leseni wa SACCOS.

35. Maombi ya leseni.

36. Mambo ya kuzingatia katika utoaji wa leseni.

37. Kukataa kutoa leseni.

38. Kuongeza muda wa leseni.

39. Kufuta leseni.

40. Rufaa dhidi ya kufutwa kwa leseni.

41. Vikwazo vya leseni.

42. Uchapishaji wa SACCOS.

## SEHEMU YA SABA
## KUVUNJWA NA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

43. Kuvunjwa kwa Chama cha Ushirika.

44. Uteuzi wa mfilisi.

45. Uwezo wa mfilisi.

46. Uwezo wa Mkurugenzi kusimamia ufilisi.

47. Kupokea na kuthibitisha madai dhidi ya Chama cha Ushirika.

48. Uhifadhi wa vitabu na kumbukumbu.

## SEHEMU YA NANE
## UKAGUZI WA HESABU, UCHUNGUZI NA UKAGUZI WA KAWAIDA WA VYAMA VYA USHIRIKA


49. Kutunza hesabu na kumbukumbu.

50. Ukaguzi wa hesabu.

51. Kuidhinisha ripoti ya Mkaguzi na taarifa za fedha.

52. Mkaguzi kupoteza sifa ya kutekeleza majukumu yake.

53. Uteuzi wa Mkaguzi.

54. Kuondolewa kwa Mkaguzi.

55. Haki ya kupata taarifa.

56. Indhari ya kosa.

57. Uchunguzi wa Mkurugenzi.

58. Ukaguzi wa kawaida wa vitabu vya Chama cha Ushirika kinachodaiwa.

59. Gharama za uchunguzi na ukaguzi wa kawaida.

60. Ukaguzi wa kushtukiza.


## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO


61. Muhuri rasmi.

62. Kuwasilisha ripoti ya mwaka.

63. Uwezo wa kutunga Sheria ndogo na maudhui yake.

64. Kosa linalohusiana na usajili au leseni.

65. Makosa ya jumla na adhabu.

66. Ada.

67. Waziri anaweza kufanya mapitio ya faini na ada.

68. Uwezo wa Waziri kutunga Kanuni.

69. Kufuta na kubakiza.

SHERIA NAM 15 YA 2018

NIMESAINI

{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

31 Disamba, 2018

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA NAM. 4 YA MWAKA 1986 NA KUTUNGA SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA ZANZIBAR YA MWAKA 2018 AMBAYO INAWEKA UTARATIBU WA UUNDAJI NA UENDESHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar ya mwaka 2018 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika kwa aina zote za Vyama vya Ushirika vinavyofanya kazi Zanzibar.

Ufafanuzi.

**3.** Kwa madhumuni ya Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Chama Kikuu" maana yake ni muungano wa Vyama vya Ushirika Zanzibar;

"Sheria ndogo" maana yake ni Kanuni zilizoidhinishwa na kukubaliwa na wanachama wa Chama cha Ushirika kilichosajiliwa kusimamia mambo yake;

"Mahakama" maana yake ni Mahakama Kuu ya Zanzibar;

"Chama cha Ushirika" maana yake ni muungano wa watu ambao wameungana pamoja kwa hiari, kwa lengo la kufikia mahitaji yao ya pamoja kupitia uundaji wa taasisi inayoendeshwa kidemokrasia na ambao wanachangia kiusawa katika mtaji unaohitajika kwa ajili ya kuunda taasisi hiyo na ambao wanakubali faida na hasara kutokana na shughuli wanazoshiriki kikamilifu, na kusajiliwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Misingi ya Ushirika" inajumuisha:

(a) uanachama wa hiari na ulio wazi;

(b) uendeshaji wa kidemokrasia wa wanachama;

(c) ushiriki wa Wanachama katika shughuli za kiuchumi;

(d) uhuru na kujitegemea;

(e) elimu, mafunzo na habari;

(f) mashirikiano miongoni mwa Vyama vya Ushirika; na

(g) kuijali jamii;

"Vigezo vya Ushirika" vinajumuisha:

(a) kujitegemea;

(b) uwajibikaji binafsi;

(c) demokrasia;

(d) usawa;

(e) haki na mshikamano ; na

(f) vigezo vya maadili:

(i) uaminifu;

(ii) uwazi;

(iii) uwajibikaji kwa jamii na kuwajali wengine;

"Mkaguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kufanya ukaguzi wa Chama cha Ushirika kama ilivyoelezewa katika kifungu cha 53 cha Sheria hii na inajumuisha Mkaguzi Binafsi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika kama inavyoelezwa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria hii;

"Mgogoro" maana yake ni kutokukubaliana, kutokufahamiana au mgongano wa kimaslahi katika mambo ya kisheria au maudhui baina ya wahusika katika mgogoro ambao utatuzi wake unasubiri maumuzi ya Mkurugenzi, Waziri au Mahakama;

"Mgao"maana yake ni sehemu ya pato lisilojumuisha dhima ya Chama cha Ushirika inayogaiwa miongoni mwa Wanachama kwa mujibu wa ushiriki wao katika miamala ya Chama cha Ushirika;

"Mwaka wa Fedha" maana yake ni mwaka ambao unaanza kutoka mwezi ambao Chama cha Ushirika kinasajiliwa;

"Mkutano Mkuu wa Kwanza" maana yake ni mkutano wa kwanza wa Wanachama wote unaofanyika baada ya kusajili Chama cha Ushirika;

"Mwanachama" maana yake ni mtu ambaye anamiliki hisa ndani ya Chama cha Ushirika;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na mambo ya Vyama vya Ushirika;

"Chama cha Ushirika cha Kati" maana yake ni Chama cha Ushirika kilichosajiliwa ambapo uwanachama wake uko wazi kwa Vyama vya Msingi tu;

"Mtu" maana yake ni mtu binafsi au taasisi inayojitegemea;

"Chama cha Ushirika cha Msingi" maana yake ni Chama cha Ushirika kilichosajiliwa ambapo wanachama wake ni watu binafsi au mkusanyiko wa watu hao;

"Kamati ya Uongozi" maana yake ni Kamati ya Uongozi ya Chama cha Ushirika.

"Katibu Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na mambo ya Vyama vya Ushirika;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"SACCOS" maana yake ni Chama cha Ushirika cha akiba na Mikopo;

"Hisa" maana yake ni mchango wa lazima unaoanzisha mtaji wa Chama cha Ushirika ambao unahalalisha umiliki wa mwanachama na kupokea na matumizi ya mgao wa faida inayotokana na ushiriki wake kwa Chama chake cha Ushirika;

"Muungano wa SACCOS" maana yake ni Chama cha Kati kilichosajiliwa kwa ajili ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHAJI NA UTAWALA WA IDARA

Uanzishaji wa Idara.

4. Kunaanzishwa Idara itakayojulikana kama Idara ya Maendeleo ya Ushirika ndani ya Wizara ambayo inahusika na mambo yanayohusiana na Vyama vya Ushirika.

Kazi za Idara

**5.**-(1) Kazi za Idara zitakuwa ni:

(a) kutoa miongozo ya kisera kwa mambo yanayohusiana na Vyama vya Ushirika;

(b) kumshauri Waziri kuhusiana na sera na mambo mengine yanayohusika katika kuimarisha Vyama vya Ushirika;

(c) kusajili aina zote za Vyama vya Ushirika, kuendeleza, kufanya ukaguzi wa hesabu, kufanya ukaguzi wa kawaida, kuchunguza, na kutoa ushauri wa kiutaalamu kwa Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(d) kuingilia kati shughuli za Vyama vya Ushirika pale maslahi ya wanachama yanapokuwa katika hali hatarishi;

(e) kujihusisha katika utatuzi wa migogoro na migongano pale inapojitokeza ndani ya Vyama vya Ushirika na katika shughuli zake;

(f) kupokea taarifa zote zinazohusiana na shughuli za Vyama vya Ushirika;

(g) kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinafuata matakwa ya Sheria hii, Taratibu na Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, kuzingatia vigezo na misingi ya Ushirika na kufuata misingi ya utawala bora ndani ya Vyama vya Ushirika;

(h) kutoa huduma zilizowekwa kwa ajili ya kusaidia katika uundaji, utayarishaji na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika;

(i) kutoa ushauri wa kitaalamu kwa aina zote za Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa katika kusimamia Vyama vya Ushirika;

(j) kuimarisha na kuwezesha upatikanaji wa elimu kwa viongozi, wanachama na wafanyakazi wa Vyama vya Ushirika;

(k) kuhakikisha uendeshaji wa kiufanisi na kitaalamu wa shughuli za Vyama vya Ushirika; na

(l) kusimamia utendaji wa jumla wa shughuli za Vyama vyote vya Ushirika kama ilivyoainishwa chini ya Sheria hii na Kanuni zake.

(2) Katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii, Idara itaendeleza kadri inavyowezekana, mfumo wa mashauriano na ushirikiano na Wizara, taasisi za Serikali au vyombo vyovyote binafsi au vya Serikali vilivyoanzishwa chini ya sheria nyengine zilizoandikwa.

Uteuzi wa Mkurugenzi.

**6.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi atakuwa pia ni Mrajisi wa Vyama vya Ushirika.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau Shahada ya Kwanza katika fani ya Usimamizi wa Ushirika na Hesabu, Utawala wa Biashara, Sheria, Maendeleo ya Jamii, Shughuli za kibenki, Uchumi au Fani nyengine za taaluma zinazohusiana na hizo;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka tisa katika fani hizo; na

(d) ana maadili ya kiwango cha juu.

Kazi na Mamlaka ya Mkurugenzi.

**7.**-(1) Mkurugenzi, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, atakuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Idara na atawajibika kwa Katibu Mkuu katika uendeshaji wa shughuli za kila siku.

(2) Mkurugenzi atasimamia utekelezaji wa kazi za Idara na atatekeleza mamlaka yote aliyopewa chini ya masharti ya Sheria hii.

(3) Mkurugenzi, katika kutekeleza kazi zake na kutumia mamlaka yake chini ya Sheria hii, anaweza kukasimu kwa maandishi kazi na mamlaka hayo kwa ofisa yeyote wa Idara au Mtu mwengine yeyote kama atakavyoona inafaa.

Ofisi ndogo Pemba.

**8.**-(1) Idara itakuwa na Ofisi ndogo Pemba ambayo itaongozwa na Mkuu wa Ofisi hiyo kama atakavyoteuliwa na Waziri.

(2) Mkuu wa Ofisi ndogo Pemba atakuwa Ofisa Dhamana wa Idara na atafanya kazi kwa kufuata maelekezo ya Mkurugenzi.

(3) Sifa za Mkuu wa Ofisi ndogo Pemba zitakuwa ni sawa na sifa za Mkurugenzi

Wafanyakazi wa Idara .

**9.**-(1) Wafanyakazi wa Idara wataajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora na wenye ufanisi kwa Idara, Katibu Mkuu anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika, kuandaa muundo wa Idara wenye vitengo au na sehemu kama itakavyohitajika.

(3) Endapo vitengo au sehemu zinaanzishwa, uteuzi wa wakuu wa vitengo au sehemu hizo utafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

## SEHEMU YA TATU
## MUUNDO, UUNDAJI NA KAZI ZA VYAMA VYA USHIRIKA

Ngazi za Vyama vya Ushirika.

**10.** Vyama vya Ushirika vitaundwa kwa mfumo wa ngazi tatu unaojumuisha:

(a) Vyama vya Ushirika vya Msingi;

(b) Vyama vya Ushirika vya Kati; na

(c) Chama Kikuu cha Ushirika.

Uundaji wa Chama cha Ushirika cha Msingi.

**11.**-(1) Chama cha Ushirika cha Msingi kimoja au zaidi kinaweza kuundwa ndani ya Shehia, Wadi yoyote au Jimbo chenye shughuli imara za kiuchumi ;

(2) Chama cha Ushirika cha Msingi kitaundwa na watu saba au zaidi;

(3) Vyama vya Ushirika vya Msingi vinavyohusiana na Akiba na Mikopo, vitaundwa na watu mia moja na hamsini au zaidi.

(4) Mtu atakuwa na sifa chini ya kifungu hiki, ikiwa mtu huyo:

(a) ni mkaazi wa eneo ambalo Chama cha Ushirika kipo;

(b) amefikia umri wa miaka kumi na nane na mwenye akili timamu;

(c) anafanya biashara au kazi inayohusiana na lengo la Chama cha Ushirika;

(d) ana mahitaji yanayofanana ambayo Chama cha Ushirika kinadhamiria kuyafikia;

(e) ana uwezo wa kulipa ada na kumiliki hisa; na

(f) ana sifa nyengine yoyote iliyoainishwa katika Sheria ndogo za Chama cha Ushirika.

**(5)** Mkurugenzi anaweza kushauri kuhusiana na aina ya Vyama vya Ushirika vinavyoweza kuundwa ndani ya Shehia au Jimbo.

Kazi za Chama cha Ushirika cha Msingi.

**12.** Chama cha Ushirika cha Msingi kitakuwa na kazi za:

(a) kukidhi mahitaji ya wanachama na kuinua hali za maisha za wanachama wake;

(b) kutoa huduma za msingi kwa wanachama wake, ikijumuisha pembejeo za kilimo, kukusanya, kuhifadhi, kusarifu, kufungasha na kutafuta masoko kwa bidhaa za wanachama wake;

(c) kununua, kuhifadhi na kusambaza pembejeo na rasilimali nyengine kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiuchumi za Chama cha Ushirika;

(d) kuratibu shughuli zote za kiuchumi za Chama cha Ushirika;

(e) kutayarisha mipango ya kiuchumi ya Chama cha Ushirika;

(f) kupanga na kutoa elimu na mafunzo kwa wanachama, viongozi na wafanyakazi wa Chama cha Ushirika; na

(g) kutekeleza shughuli za kijamii na kiuchumi zilizoainishwa na Sheria zao ndogo.

Uundaji wa Chama cha Ushirika cha Kati.

**13.** Chama cha Ushirika cha Kati kitaundwa angalau na vyama vitano vya Ushirika vya Msingi vilivyosajiliwa baada ya kuridhiwa na wanachama katika Mkutano Mkuu.

Kazi za Chama cha Ushirika cha Kati.

**14.** Chama cha Ushirika cha Kati kitakuwa na kazi za:

(a) kuwasaidia na kuwawakilisha wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Msingi;

(b) kumsaidia Mkurugenzi katika hatua za usajili wa Vyama vya Ushirika vya Msingi;

(c) kukusanya takwimu na taarifa kutoka katika Vyama vya Ushirika vya Msingi kuhusu uzalishaji, usambazaji wa pembejeo na upatikanaji wa masoko kwa mipango ya maendeleo;

(d) kutoa huduma za ushauri kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika kwenye masuala yanayohusiana na ununuzi wa jumla, uhifadhi wa pamoja, mapatano ya bei na udhibiti wa ubora;

(e) kuwezesha uendeshaji wa Vyama vya Ushirika vya Msingi na kuhamasisha uwekezaji wenye tija kwa wanachama;

(f) kuongoza, kusimamia na kuratibu shughuli za Vyama vya Ushirika wanachama;

(g) kutoa dhamana na huduma za hesabu na ukaguzi kwa Vyama vya Ushirika wanachama ;

(h) kuanzisha na kuendesha Mfuko Mkuu wa Fedha kwa ajili ya kuendeleza biashara na huduma za usimamizi kwa Vyama vya Ushirika wanachama;

(i) kuwakilisha maslahi ya Vyama vya Ushirika wanachama katika Chama Kikuu cha Ushirika na kuimarisha sauti zao kupitia utetezi na ushawishi;

(j) kutoa huduma nyengine zozote kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi kama zitakavyoainishwa katika sheria ndogo; na

(k) kufanya usuluhishi na utatuzi wa migogoro kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika.

Uundaji wa Chama Kikuu cha Ushirika.

**15.** Kutakuwa na Chama Kikuu cha Ushirika ambacho kitaundwa kwa angalau Vyama vya Ushirika vya Kati vitano baada ya kuridhiwa na wanachama katika Mkutano Mkuu.

Kazi za Chama Kikuu cha Ushirika.

**16.** Chama Kikuu cha Ushirika kitakuwa na kazi za:

(a) kumsaidia Mkurugenzi katika hatua ya usajili wa Chama cha Ushirika cha Kati;

(b) kutetea uwepo wa harakati imara za maendeleo ya Vyama vya Ushirika;

(c) kuwezesha uendeshaji wa miungano ya Vyama vya Ushirika, na kuhamasisha uwekezaji mzuri wa Vyama vya Ushirika vya Kati;

(d) kutoa huduma kwa Vyama vya Ushirika vya Kati kama zinavyoainishwa na sheria ndogo za Chama cha Ushirika Kikuu;

(e) kutoa huduma za ushauri kwa mwanachama wa Vyama vya Ushirika vya Kati;

(f) kutoa huduma zilizowekwa ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi na kuendana na utendaji wa shughuli za wanachama wake kwa kuweka mfumo mmoja wa utunzaji kumbukumbu, hesabu na ukaguzi na taratibu nyengine kwa Chama cha Ushirika cha Kati;

(g) kuwakilisha Vyama wanachama wake katika mapatano ya pamoja;

(h) kuwakilisha Vyama wanachama wake katika harakati za Vyama vya Ushirika kimataifa;

(i) kuanzisha na kuendesha Mfuko Mkuu wa Fedha kwa ajili ya kuendeleza biashara na huduma za usimamizi za Vyama vya Ushirika wanachama wao; na

(j) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo imeainishwa katika sheria ndogo za Chama Kikuu cha Ushirika ambazo kwa maoni yake inaendana na au ni sehemu ya kazi zake chini ya kifungu hiki.

## SEHEMU YA NNE
## USAJILI WA VYAMA VYA USHIRIKA

Usajili wa Vyama vya Ushirika.

**17.**-(1) Chama cha Ushirika kitasajiliwa na Mkurugenzi chini ya masharti ya Sheria hii.

(2) Mkurugenzi, wakati wa kusajili Chama cha Ushirika chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, pamoja na mambo mengine, atazingatia misingi na vigezo vya ushirika vinavyokubalika vilivyoainishwa chini ya Sheria hii.

(3) Taratibu za usajili zitaelezwa katika Kanuni zitakazotungwa na Waziri chini ya Sheria hii.

Taratibu za kuomba usajili.

**18.**-(1) Chama cha Ushirika, kwa namna itakavyoelezwa chini ya Kanuni, kitaomba kwa Mkurugenzi kusajiliwa chini ya Sheria hii.

(2)Baada ya kupokea maombi ya usajili, Mkurugenzi, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, atathibitisha maombi na endapo ataridhika, atasajili Chama cha Ushirika kwa kukiingiza katika Daftari la Vyama vya Ushirika lililowekwa kwa ajili hiyo.

(3) Baada ya kuingizwa Chama cha Ushirika katika Daftari, Mkurugenzi atatoa Hati katika namna iliyoelezwa chini ya Kanuni ambayo itakuwa ni ushahidi wa kuthibitisha kuwa Chama kimesajiliwa.

Athari ya usajili.

**19.** Chama cha Ushirika kilichosajiliwa kutoka tarehe ambayo kimesajiliwa kitakuwa ni chombo kinachojitegemea chenye urithi wa kuendelea na muhuri wake na kwa jina lake, kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kumiliki, kununua, kuondosha mali inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kupokea au kutoa mikopo, kukopa au kukopesha fedha;

(d) kuingia katika mikataba; na

(e) kufanya au kutekeleza mambo mengine yote au vitu kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii au sheria zake ndogo.

Kukataa kusajili.

**20.** Mkurugenzi anaweza, endapo ataridhika kwamba Chama cha Ushirika kimeshindwa kutimiza masharti ya usajili yaliyoelezwa, au ataridhika kwamba Chama cha Ushirika hicho hakipo au kimeshindwa kutimiza masharti mengine yaliyoelezwa chini ya Sheria hii, kukataa kukisajili Chama cha Ushirika hicho, na atakijuilisha kwa maandishi sababu za kukataa huko.

Rufaa dhidi ya kukataa usajili.

**21.**-(1) Mtu ambaye hakuridhishwa na maamuzi ya Mkurugenzi chini ya kifungu cha 20 cha Sheria hii, anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku kumi na nne baada ya maamuzi hayo kutolewa.

(2) Waziri, ndani ya siku ishirini na moja, kutoka tarehe aliyopokea rufaa, atatoa maamuzi ya rufaa.

Kufuta usajili.

**22.** Mkurugenzi anaweza kufuta usajili wa Chama chochote cha Ushirika endapo akiridhika kwamba, Chama cha Ushirika kina yafuatayo:

(a) kina wanachama chini ya idadi inayotakiwa kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) hakijafanya miamala ya kibiashara katika kipindi cha miezi sita baada ya ukaguzi wa kawaida, ukaguzi wa hesabu na huduma za kiushauri zinazotolewa kwa Vyama vya Ushirika;

(c) hakina nia tena kuendelea kufanya shughuli yoyote iliyoainishwa katika sheria zake ndogo;

(d) kimejivunja chenyewe;

(e) kimesita kuwa ni Chama cha Ushirika kwa maana ya Sheria hii;

(f) kimeshindwa kufuata misingi na vigezo vya Chama cha Ushirika; na

(g) kimevunja masharti yoyote ya Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Rufaa dhidi ya kufuta usajili.

**23.**-(1) Chama cha Ushirika kinaweza, ndani ya siku thelathini baada ya kufutiwa usajili, kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Waziri, ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe aliyopokea rufaa, atatoa maamuzi ya rufaa.

## SEHEMU YA TANO
## MUUNDO WA MTAJI, HISA NA MALI ZA CHAMA CHA USHIRIKA

Mtaji wa Chama cha Ushirika.

**24.** Vyanzo vya Mtaji wa Chama cha Ushirika vinaweza kuundwa na moja kati ya vifuatavyo:

(a) ada ya kiingilio;

(b) ada au michango ya uanachama kama ilivyoelezwa katika sheria ndogo za Chama cha Ushirika;

(c) hisa kutoka kwa wanachama na fedha inayozunguka kwa utaratibu wa mkopo;

(d) ruzuku, michango na michango mengine kutoka katika Serikali au wafadhili binafsi iliyopatikana kihalali;

(e) mikopo kutoka kwa wanachama, Vyama vyengine vya Ushirika, Benki na taasisi za kifedha za umma au binafsi kwa malengo ya kuwekeza;

(f) amana kutoka kwa wanachama na Vyama vyengine vya Ushirika;

(g) ziada baada ya mgao kwa wananchama kwa kadri walivyoshiriki, mgao ambao uliotolewa kwa mujibu masharti yaliyoelezwa na sheria ndogo za Chama cha Ushirika; na

(h) mtaji mwengine wowote halali uliopatikana kutoka katika chanzo ambacho sio kati ya vilivyotajwa chini ya kifungu hiki.

Mfuko wa Akiba wa Chama cha Ushirika.

**25.**-(1) Chama cha Ushirika kitaweka Mfuko wa Akiba ambapo ndani yake Chama hicho cha Ushirika kitaweka angalau asilimia thelathini na tano ya ziada kama ni akiba ambayo haitagawanywa kwa wanachama wake katika mwaka wa fedha.

(2) Chama cha Ushirika kinaweza kuutumia Mfuko uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kwa namna iliyoainishwa katika kifungu cha 26 cha Sheria hii.

(3) Mfuko wa Akiba wa Chama cha Ushirika utasimamiwa na Mkurugenzi au mtu mwengine yeyote aliyemuidhinisha kwa kufuata masharti, kupitia hesabu za mwaka zilizokaguliwa.

Madhumuni ya Mfuko wa Akiba.

**26.**-(1) Mfuko wa Akiba unaweza kutumika kwa:

(a) kuwekeza katika hesabu ya amana ya muda maalumu katika taasisi inayotambulika rasmi au katika Benki inayofanya kazi Zanzibar;

(b) kutekeleza wajibu wa kisheria wa Chama cha Ushirika;

(c) kuwekeza katika majengo;

(d) kuwekeza katika kuendeleza huduma muhimu kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wanachama;

(e) kusaidia matumizi muhimu kama vile vifaa au huduma za uendeshaji;

(f) kuwekeza katika dhamana za Serikali na hati fungani;

(g) kuwekeza katika Chama cha Ushirika kinachofanya vizuri; na

(h) kutumia fursa katika uwekezaji wowote halali kwa ustawi wa Chama cha Ushirika.

(2) Chama cha Ushirika, kabla ya kutumia Mfuko wa Akiba wa wanachama, lazima kiwe na azimio maalumu la Mkutano Mkuu kwa madhumuni hayo.

Masharti ya kugawa ziada.

**27.**-(1) Chama cha Ushirika kitagawa miongoni mwa wanachama wake ziada yoyote iliyopatikana inavyostahiki;

(2) Chama cha Ushirika hakitagawa au kulipa sehemu yoyote ya faida yake kabla **ya** mezania kukaguliwa na kuidhinishwa na Mkurugenzi baada ya azimio la wanachama katika Mkutano Mkuu.

(3) Chama cha Ushirika kitagawa pia miongoni mwa wanachama wake, ziada yoyote iwapo kitatenga na kuingiza katika Mfuko wa Akiba angalau asilimia thelathini na tano ya faida safi katika mwaka wowote.

(4) Malipo kutoka kwa faida iliyobakia na faida yoyote ya mwaka uliopita iliyopo kwa ajili ya kugawanywa, yanaweza kufanywa kwa wanachama kwa kiwango na chini ya masharti kama yatakavyoelezwa katika Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii au sheria ndogo za Chama cha Ushirika.

Mikopo na dhamana iliyoruhusiwa na iliyokatazwa.

**28.**-(1) Chama cha Ushirika kinaweza kutoa msaada wa kifedha kwa njia ya mkopo au utoaji wa dhamana kwa:

(a) mwanachama yeyote katika shughuli zake za kawaida ikiwa ukopeshaji wa fedha ni sehemu ya shughuli za kawaida za Chama hicho cha Ushirika;

(b) mtu yeyote ambaye amefanya matumizi au atafanya matumizi kwa niaba ya Chama cha Ushirika; na

(c) Waajiriwa wa Chama cha Ushirika au miongoni mwa wanachama wake kuwawezesha au kuwasaidia kununua au kujenga majengo ya biashara au ya makaazi.

(2) Chama cha Ushirika hakitatoa msaada wa kifedha kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, moja kwa moja au vyenginevyo ikiwa kuna sababu za msingi za kuamini kwamba:

(a) Chama cha Ushirika, baada ya kutoa msaada wa kifedha hakitaweza kulipa dhima zake zilizopo; au

(b) Thamani inayotambulika ya mali za Chama cha Ushirika, baada ya kutoa msaada wa kifedha, itakuwa chini ya jumla ya dhima zake, mtaji wa hisa na akiba.

(3) Katika kuamua thamani inayotambuliwa ya mali za Chama cha Ushirika iliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, kiwango cha msaada

wowote wa kifedha kwa njia ya mkopo na kwa njia ya mali za rehani au iliyozuiliwa kwa ajili ya kupata dhamana hazitajumuishwa.

Uwekezaji wa Fedha.

**29.**-(1) Chama cha Ushirika kilichosajiliwa kinaweza kuwekeza au kuweka fedha zake katika uwekezaji ufuatao:

(a) katika Benki za Serikali na mifuko mengine ya Serikali;

(b) amana za Serikali, dhamana na Benki za Biashara;

(c) katika hisa au dhamana za Chama cha Ushirika chochote kilichosajiliwa;

(d) Benki yoyote au taasisi inayoendesha shughuli za kibenki iliyoidhinishwa na Waziri kwa madhumuni hayo; au

(e) katika mfumo mwengine wowote ulioruhusiwa na Kanuni na kuidhinishwa na Waziri.

(2) Uwekezaji au uwekaji wa amana yoyote uliofanywa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, ambao ingelikuwa halali kama Sheria hii ingelikuwa inatumika kwa wakati huo, unaridhiwa na kuthibitishwa.

Matumizi mabaya ya mali ya Chama cha Ushirika.

**30.** Mtu ambaye:

(a) ana mali kwa njia ya udanganyifu au anajimilikisha mali yoyote iliyosajiliwa ya Chama cha Ushirika;

(b) ana mali yoyote katika himaya yake ya Chama cha Ushirika kilichosajiliwa, ameizuwia au anaitumia visivyo; au

(c) kwa makusudi anatumia sehemu yoyote ya mali iliyotajwa katika aya (a) au (b) ya kifungu hiki, kwa madhumuni mbali na yale yaliyoelezwa au yaliyoelekezwa katika Sheria ndogo za Chama cha Ushirika na yakaidhinishwa na Sheria hii, mtu huyo, atakapolalamikiwa na Chama cha Ushirika au mwanachama yeyote aliyeidhinishwa au kamati yoyote ya Chama cha Ushirika, au wajumbe wa Kamati ya Uongozi,

ametenda kosa na akipatikana na hatia, analazimika kulipa kiwango kilichotumika visivyo, na faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kifungo kwa kipindi cha miezi sita au vyote viwili faini na kifungo.

## SEHEMU YA SITA
## VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO

Matumizi ya Sehemu hii.

**31.**-(1) Sehemu hii inatumika kwa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS).

(2) Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo vitafuata masharti ya Sehemu hii, masharti mengine husika ya Sheria hii na Kanuni za SACCOS.

Madhumuni ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.

**32.** Kwa madhumuni ya Sehemu hii, Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo ni taasisi ya kifedha inayomilikiwa na wanachama ambapo lengo lake ni kuhamasisha rasilimali za kifedha za wanachama kupitia akiba, hisa na amana kwa ajili ya kuwakopesha wanachama kwa kiwango cha riba na faini zilizokubaliwa na kuridhiwa; SACCOS itatoa mtaji kwa wanachama wawekeze katika miradi ya kijamii na kiuchumi.

Mahitaji ya Sheria ndogo.

**33.** Kwa madhumuni ya Sehemu hii, kila SACCOS itaandaa Sheria ndogo ambazo zitaelezea namna zitakavyounda uongozi, uendeshaji na usimamizi kuhusiana na mambo yanayoelezwa katika Kanuni zinazotungwa chini ya Sheria hii.

Ukataji leseni wa SACCOS.

**34.** Chama chochote cha Ushirika kitaendesha shughuli za SACCOS kwa maana iliyokusudiwa katika Sehemu hii ikiwa:

(a) SACCOS imesajiliwa chini ya masharti ya Sheria hii; na

(b) ina leseni halali iliyotolewa chini ya Sheria hii.

Maombi ya leseni.

**35.**-(1) SACCOS itaomba leseni kwa Mkurugenzi kwa utaratibu utakaoelezwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Maombi yanayofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yataambatana na:

(a) nakala ya Hati ya Usajili na Sheria ndogo za SACCOS;

(b) ushahidi wa kwamba SACCOS imetimiza masharti ya mtaji yaliyoelezwa katika Kanuni;

(c) taarifa zinazohusiana na anuwani ya biashara;

(d) ada iliyoelekezwa;

(e) ripoti ya mwaka ya SACCOS inayojumuisha:

(i) hali ya utendaji wa SACCOS;

(ii) uwanachama na mtaji wa hisa;

(iii) orodha ya wajumbe wa Kamati ya Uongozi;

(iv) mpango wa fedha;

(v) timu ya uongozi;

(vi) ripoti ya fedha na ukaguzi;

(vii) uchambuzi wa vihatarishi na jinsi ya kuvikabili;

(viii) kumbukumbu za vikao; na

(ix) taarifa nyengine kama itakavyoelekezwa na Mkurugenzi.

(3) SACCOS ambayo ilikuwepo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, inapewa muda wa miezi kumi na mbili ya kwenda kujisajili upya kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Mambo ya kuzingatia katika utoaji wa leseni.

**36.**-(1) Mkurugenzi atazingatia kila ombi lililofanywa chini ya kifungu cha 35 na anaweza, ikiwa ataridhirika kwamba muombaji ametimiza masharti ya Sheria hii, kutoa leseni kwa muombaji baada ya kulipa ada iliyoelezwa.

(2) Mkurugenzi, baada ya muombaji kulipa ada iliyoelezwa, atatoa leseni kwa SACCOS kwa ajili ya kuendesha shughuli yake.

Kukataa kutoa leseni.

**37.**-(1) Mkurugenzi anaweza kukataa kutoa leseni kwa SACCOS yoyote, ikiwa masharti chini ya kifungu cha 35 hayakutimizwa.

(2) SACCOS inaweza kukata rufaa kwa Waziri itakapotokea kukataliwa kupewa leseni, ndani ya siku kumi na nne baada ya kupewa taarifa ya kukataliwa huko.

(3) Waziri anaweza kubatilisha maamuzi ya Mkurugenzi iwapo:

(a) Mkurugenzi ameshindwa kufuata utaratibu unaotakiwa katika kutoa maamuzi;

(b) maamuzi ya Mkurugenzi yameenda kinyume na Sheria au Kanuni; na

(c) kwa kuzingatia mapitio ya kumbukumbu, Mkurugenzi amekosea katika kufanya tathmini ya taarifa sahihi, au ametumia mamlaka yake vibaya katika kutoa maamuzi.

(4) Mkurugenzi kwa kushauriana na Waziri, ataandaa miongozo itakayoelezea masharti ya ziada kutimizwa kabla ya utoaji wa leseni kwa SACCOS.

Kuongeza muda wa leseni.

**38.**-(1) Kila SACCOS itaongeza muda wa leseni na italipa ada ya kuongeza muda kwa kiwango na katika kipindi kama itakavyoelezewa katika Kanuni.

(2) SACCOS ambayo itashindwa kuongeza muda wa leseni katika muda ulioainishwa pamoja na hatua yoyote itakayochukuliwa na Mkurugenzi, itawajibika kulipa faini kama Mkurugenzi atakavyoeleza.

(3) SACCOS ambayo inashindwa kuanza shughuli zake ndani ya miezi sita baada ya kupewa leseni chini ya Sheria hii, ikiwa bado ina nia ya kuendesha biashara hiyo itafanya maombi mapya chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii.

Kufuta leseni.

**39.**-(1) Mkurugenzi anaweza, kutoa taarifa ya maandishi kwa SACCOS, kufuta leseni ikiwa SACCOS hiyo:

(a) imesita kuendesha biashara yake, au inaelekea kufilisika au inafungwa au vyenginevyo inavunjwa au imefutiwa usajili wake chini ya Sheria hii;

(b) inashindwa kufuata masharti ya Sheria hii, au taratibu zozote, kanuni, amri au maelekezo yaliyotolewa ndani ya Sheria hii au sharti lolote la leseni;

(c) haimiliki angalau asilimia hamsini ya mtaji wa hisa zilizolipwa;

(d) kwa kujua imetenda makosa makubwa ya jinai au udanganyifu ambayo yatapelekea kusababisha kufilisika, matumizi makubwa ya mali na mapato au vyenginevyo inaweza kudhoofisha amana za SACCOS au kwa kiwango kikubwa kuathiri maslahi ya wanachama wa SACCOS.

(2) Mkurugenzi, kabla ya kufuta leseni, ataipa SACCOS taarifa ya maandishi ya siku kumi na nne kuhusiana na dhamira hiyo, na atazingatia hoja zozote zitakazowasilishwa kwa maandishi na SACCOS ndani ya kipindi hicho kabla ya kufutwa leseni hiyo.

(3) Mkurugenzi atawezesha jina la kila SACCOS ambayo leseni yake imefutwa chini ya kifungu hiki kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na angalau gazeti moja linalosambazwa kwa kiwango kikubwa Zanzibar.

(4) Endapo leseni ya SACCOS imefutwa, SACCOS haitostahiki kurejeshewa ada yoyote ya leseni kuhusiana na kipindi chochote kilichobakia cha matumizi ya leseni hiyo.

Rufaa dhidi ya kufutwa kwa leseni.

**40.**-(1) SACCOS ambayo haikuridhishwa na maamuzi ya Mkurugenzi inaweza, ndani ya siku thelathini baada ya kufutwa leseni hiyo, kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Waziri, ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe ya kupokea rufaa hiyo, atatoa maamuzi ya rufaa.

Vikwazo vya leseni.

**41.**-(1) Endapo itaonekana na Mkurugenzi kwamba, kuna sababu za msingi za kufuta leseni, lakini mazingira ya ufutaji wa leseni hiyo hayatokuwa na manufaa au sio ya haki kwa wanachama, Mkurugenzi anaweza kuweka vikwazo kwa leseni hiyo kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

(2) Leseni inaweza kuwekewa kikwazo kwa kuweka:

(a) ukomo kwa muda wa leseni kwa kipindi kisichozidi miezi sita; au

(b) masharti mengine ya ziada kwa kulinda maslahi ya waliyoweka amana kama Mkurugenzi atakavyoona inafaa.

Uchapishaji wa SACCOS.

**42.**-(1) Mwamvuli wa SACCOS utawezesha kuchapishwa orodha ya SACCOS zote kila mwaka angalau katika gazeti moja linalosambazwa kwa kiwango kikubwa Zanzibar.

(2) Utolewaji wa taarifa za SACCOS zitajumuisha:

(a) machapisho ya SACCOS;

(b) mahitaji ya kiwango cha chini cha mtaji wa hisa kwa SACCOS;

(c) kiwango cha chini cha mali zilizopo;

(d) shughuli zinazokatazwa;

(e) eneo la biashara;

(f) maombi ya huduma za mkopo kutoka vyanzo vya nje; na

(g) uwekezaji katika SACCOS.

## SEHEMU YA SABA
## KUVUNJWA NA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Kuvunjwa kwa Chama cha Ushirika.

**43.**-(1) Chama cha Ushirika kinaweza kuvunjwa:

(a) kwa azimio maalum la angalau theluthi mbili ya wanachama wake; na

(b) kupitia Mahkama kwa maombi ya angalau nusu ya idadi ya wanachama wa Chama cha Ushirika.

(2) Chama cha Ushirika kinaweza kuvunjwa kutokana na sababu zifuatazo:

(a) Chama cha Ushirika hakiwezi kulipa madeni yake;

(b) hakuna uwezekano kwamba kitaweza kuendesha shughuli zake kama Chama cha Ushirika imara; na

(c) endapo ikionekana kuwa ni haki na busara kufanya hivyo.

(3) Endapo Chama cha Ushirika kinavunjwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) (b) cha kifungu hiki, Mahkama, katika kuzingatia maombi, inaweza:

(a) kuakhirisha usikilizaji wa maombi hayo kwa masharti au bila ya masharti; au

(b) kabla ya kukubali au kukataa ombi, kuweka masharti ya muda au kutoa amri nyengine kama itakavyoona inafaa.

Uteuzi wa mfilisi.

**44.**-(1) Endapo Chama cha Ushirika kinavunjwa kwa mujibu wa kifungu cha 43(1) (a), Mkurugenzi atamteua mtu mweledi kuwa mfilisi wa Chama cha Ushirika, na mali zote na dhima za Chama cha Ushirika zitakuwa chini ya mfilisi kutoka tarehe iliyoanzia uteuzi wake.

(2) Mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Uwezo wa mfilisi.

**45.**-(1) Mfilisi atakuwa na uwezo wa:

(a) kufungua na kutetea mashauri na mienendo mengine ya kisheria kwa niaba ya Chama cha Ushirika kwa jina lake au ofisi na kuhudhuria Mahakamani kama Mdai yeye mwenyewe kwa niaba ya Chama cha Ushirika;

(b) kuamua mchango utakaotolewa na wanachama kuhusiana na mali za Chama cha Ushirika;

(c) kuchunguza madai yote dhidi ya Chama cha Ushirika na kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kuamua masuala ya vipaumbele yanayojitokeza baina ya wadai;

(d) kuamua kila baada ya muda ni watu gani na kwa kiwango cha uwiano gani gharama za ufilisi zitalipwa;

(e) kuchukua vitabu, nyaraka na mali za Chama cha Ushirika;

(f) kutathmini na kuchunguza dai lolote ambalo Chama cha Ushirika linaweza kuwa nalo dhidi ya mtu yeyote;

(g) kuamua dhima kwa gharama za ufilisi; na

(h) kutoa maelekezo kuhusiana na ukusanyaji na ugawaji wa mali za Chama cha Ushirika na uondoshaji wa vitabu na nyaraka za Chama cha Ushirika kama atakavyoona kuwa ni muhimu kwa ufungaji wa shughuli za Chama cha Ushirika.

(2) Mfilisi, katika kutumia uwezo wake, atafuata masharti ya Sheria husika inayohusiana na ufilisi.

Uwezo wa Mkurugenzi kusimamia ufilisi.

**46.** Mkurugenzi, kuhusiana na mfilisi kutumia uwezo wake chini ya kifungu cha 45 cha Sheria hii, anaweza:

(a) kukataa au kubadilisha amri yoyote iliyotolewa na mfilisi na kutoa amri nyengine mpya inayohitajika;

(b) kumuondosha mfilisi madarakani;

(c) kuvihitaji vitabu, nyaraka na mali za Chama cha Ushirika;

(d) kwa amri ya maandishi, kuweka mipaka ya uwezo wa mfilisi chini ya masharti ya Sheria hii;

(e) kutaka hesabu ziwasilishwe kwake na mfilisi;

(f) kutoa amri ya maslahi ya mfilisi;

(g) kulipeleka jambo lolote la mgogoro baina ya mfilisi na mtu yeyote wa tatu kwa ajili ya usuluhishi ikiwa mtu huyo atayaridhia kwa maandishi maamuzi yatakayotolewa kutokana na mgogoro huo.

Kupokea na kuthibitisha madai dhidi ya Chama cha Ushirika.

**47.**-(1) Mtu ambaye ana dai, lisilokuwa dai dhidi ya Mfuko wa wanachama, dhidi ya Chama cha Ushirika kinachovunjwa, atawasilisha Hati ya Kiapo kwa mfilisi kwa:

(a) kubainisha kiwango cha dai pamoja na nyaraka nyengine zitakazosaidia; na

(b) kujumuisha taarifa zozote zilizoelezwa kuhusiana na dai hilo.

(2) Dai lililotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, litawasilishwa ndani ya siku tisini za uchapishaji wa tangazo la uteuzi wa mfilisi.

(3) Ikitokezea ucheleweshaji, katika muda uliowekwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) ya kipindi chengine cha siku thelathini za ziada kwa ridhaa ya Mkurugenzi.

(4) Mfilisi anaweza:

(a) kukubali au kukataa dhima ya chama cha ushirika kwa kiwango cha dai kilichotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki; au

(b) kukubali dhima ya Chama cha Ushirika kwa sehemu yoyote ya kiwango hicho.

(5) Mtu ambaye hakuridhishwa na maamuzi ya mfilisi chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki anaweza, ndani ya siku thelathini baada ya kupewa taarifa ya maamuzi hayo, kukata rufaa kwa Waziri.

(6)Mwanachama ambaye halikubali dai dhidi ya Mfuko wa wanachama kuendelea, atamtaarifu mfilisi kwa maandishi.

(7) Masharti ya kifungu hiki hayamzuwii mdai kuthibitisha dai lake katika Mahakama yenye mamlaka.

Uhifadhi wa vitabu na kumbukumbu.

**48.** Mfilisi atamkabidhi Mkurugenzi vitabu vyote na kumbukumbu za Chama cha Ushirika, na Mkurugenzi anaweza baada ya kipindi cha miaka miwili tangu kuondolewa jina la Chama cha Ushirika kwenye daftari la kumbukumbu, kuwezesha vitabu hivyo na kumbukumbu kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria zinazosimamia masuala ya nyaraka.

## SEHEMU YA NANE
## UKAGUZI WA HESABU, UCHUNGUZI NA UKAGUZI WA KAWAIDA WA VYAMA VYA USHIRIKA

Kutunza hesabu na kumbukumbu.

**49.**-(1) Chama cha Ushirika kitaweka vitabu vya hesabu na vitabu vyengine kwa madhumuni ya kurekodi miamala yote inayohusiana na uendeshaji, fedha, shughuli na mali, si zaidi ya miezi mitatu ya awali ya mwaka mpya wa fedha.

(2) Chama cha Ushirika:

(a) kitahakikisha kwamba malipo yote yanayoidhinishwa na kufanywa kwa usahihi na kwamba usimamizi mzuri unaendelezwa kwenye mapato yake, matumizi, mali na dhima;

(b) kitatunza hesabu zote na kumbukumbu kwa namna ambayo vitaonyesha wazi hali ya kifedha ya Chama cha Ushirika na kwamba mdhibiti wa ndani au mkaguzi anaweza kuvipata katika muda wote muafaka; na

(c) kitahakikisha kwamba hesabu zote kuhusiana na mwaka wa fedha husika zinafungwa na kukaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na Kanuni.

Ukaguzi wa hesabu.

**50.**-(1) Mkurugenzi au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Mkurugenzi atakagua hesabu za kila Chama cha Ushirika kilichosajiliwa angalau mara moja kwa kila mwaka.

(2) Madhumuni ya ukaguzi wa hesabu ni:

(a) kuhakikisha kwamba taarifa za kifedha zinafungwa kwa mujibu wa viwango na taratibu za uhasibu zinazokubalika;

(b) kujiridhisha kwamba Chama cha Ushirika kinatunza kumbukumbu vya kutosha kwa mujibu wa masharti ya Sheria yake ndogo na Sheria hii;

(c) kutoa taarifa kwa ujumla kama mali na huduma za Chama cha Ushirika zinasimamiwa vizuri na shughuli za Chama cha Ushirika zinaendeshwa kwa mujibu wa misingi ya Ushirika; na

(d) kutoa taarifa kuhusiana na jambo jengine lolote ambalo wakaguzi wanatakiwa kutoa taarifa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ndogo za Vyama vya Ushirika.

Kuidhinisha ripoti ya Mkaguzi na taarifa za fedha.

**51.**-(1) Chama cha Ushirika kinaweza kusambaza rasimu ya ripoti ya fedha zilizokaguliwa kwa wanachama wake angalau siku saba kabla ya mkutano mkuu wa mwaka.

(2) Mkutano mkuu wa mwaka utazingatia uidhinishaji wa ripoti ya Mkaguzi na taarifa za fedha.

(3) Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi, au mtu ambaye alikaimu katika mkutano huo ambapo ripoti ya Mkaguzi na taarifa za fedha ziliidhinishwa, ataweka saini ripoti ya Mkaguzi na taarifa za fedha kuthibitisha uidhinishwaji wake.

(4) Chama cha Ushirika, hakitatoa, kuchapisha au kusambaza nakala za taarifa za fedha isipokuwa taarifa hizo ziwe:

(a) zimeidhinishwa na Mkutano Mkuu na kusainiwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki; na

(b) zimeambatanishwa na ripoti ya Mkaguzi.

(5) Ripoti ya Mkaguzi na taarifa za fedha zitawekwa kwa ajili ya ukaguzi wa kawaida katika ofisi iliyosajiliwa ya Chama cha Ushirika kwa angalau siku ishirini na moja baada ya kuidhinishwa ripoti hiyo na taarifa za fedha.

(6) Kamati ya Uongozi:

(a) itawasilisha nakala ya taarifa ya fedha na ripoti ya Mkaguzi kwa Mkurugenzi ndani ya siku kumi na tano baada ya kuidhinishwa kwake; au

(b) iwapo kwa sababu yoyote Mkutano Mkuu wa mwaka unashindwa kuidhinisha taarifa za fedha na ripoti ya Mkaguzi, itamtaarifu Mkurugenzi ndani ya siku kumi na tano sababu ya kushindwa huko na hatua ya Chama cha Ushirika inayopendekeza kuchukua kukabiliana na hali hiyo.

Mkaguzi kupoteza sifa ya kutekeleza majukumu yake.

**52.** Mtu atapoteza sifa ya kuwa Mkaguzi wa Chama cha Ushirika ikiwa:

(a) Mtu huyo ana maslahi binafsi au maslahi ya kimali katika Chama cha Ushirika au maslahi yoyote katika uwekezaji wa Chama cha Ushirika au katika matawi yoyote ya Ushirika au katika shughuli zozote za wanachama wake au waajiriwa waandamizi; au

(b) katika mazingira mengine yoyote ambayo yanahusishwa na mgongano wa kimaslahi kwa mujibu wa taratibu za uhasibu.

Uteuzi wa Mkaguzi.

**53.**-(1) Chama cha Ushirika kitamteua Mkaguzi kukaguwa vitabu vya hesabu vya Chama cha Ushirika, kwa kuzingatia kwamba, uteuzi huo umeidhinishwa na Mkurugenzi.

(2) Ikiwa Chama cha Ushirika kimeshindwa kumteua Mkaguzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi anaweza kumuidhinisha mtu aliyependekezwa na Kamati ya Uongozi ya Chama cha Ushirika kukagua vitabu vyake kwa mwaka mmoja wa fedha.

(3) Muda wa Mkaguzi kutumikia nafasi yake utakuwa kama utakavyoelezwa katika Kanuni

(4) Maslahi atakayolipwa Mkaguzi yataidhinishwa na Kamati ya Uongozi.

(5) Mkaguzi wa Chama cha Ushirika atasita kushikilia nafasi yake iwapo atakufa, atajiuzulu au ataondolewa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 54 cha Sheria hii, au ameondolewa katika orodha ya wakaguzi kwa mujibu wa Sheria zinazotumika Zanzibar.

(6) Kujiuzulu kwa Mkaguzi kunaanza rasmi kutoka tarehe ambayo taarifa ya maandishi kuhusiana na kujiuzulu imepokelewa na Chama cha Ushirika, au tarehe iliyoainishwa katika kujiuzulu kwake, kutegemeana na itakayokuwa ya mwisho.

Kuondolewa kwa Mkaguzi.

**54.**-(1) Wanachama wanaweza kupitia azimio la kawaida, kumuondosha Mkaguzi katika nafasi yake.

(2) Nafasi iliyoachwa wazi kutokana na kuondolewa Mkaguzi;

(a) itajazwa katika mkutano ambao Mkaguzi huyo ameondolewa; au

(b) ikiwa haikujazwa katika mkutano, ndani ya siku thelathini za kuachwa wazi nafasi hiyo itajazwa na Kamati ya Uongozi ya Chama cha Ushirika kwa idhini ya Mkurugenzi.

(3) Mkaguzi anayeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, atatumikia nafasi yake kwa muda uliobaki wa mtangulizi wake.

Haki ya kupata taarifa.

**55.** Kwa maombi ya Mkaguzi, wanachama, Kamati ya Uongozi, waajiriwa, mawakala au Chama cha Ushirika kitatoa taarifa yoyote, maelezo, na kuwezesha

upatikanaji wa nyaraka za Chama cha Ushirika au katika matawi yake yoyote, ambapo kwa maoni ya Mkaguzi, ni muhimu kwa madhumini ya ukaguzi.

Indhari ya kosa.

**56.**-(1) Mjumbe wa Kamati ya Uongozi au muajiriwa, ambaye anafahamu kosa lolote au taarifa iliyopotoshwa katika taarifa za fedha ambapo Mkaguzi au Mkaguzi aliyepita alitoa taarifa, atamtaarifu Mkaguzi bila ya kuchelewa.

(2) Mkaguzi au Mkaguzi aliyepita wa Chama cha Ushirika ambaye amepewa taarifa, au kwa namna nyengine yoyote anafahamu, makosa yenye athari au taarifa potofu za kifedha ambazo zimeripotiwa, atalazimika kuiarifu Kamati ya Uongozi ipasavyo.

(3) Iwapo Mkaguzi au Mkaguzi aliyepita ataitaarifu Kamati ya Uongozi kuhusiana na makosa au upotovu katika taarifa za fedha kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Kamati ya Uongozi:

(a) itaandaa na kutoa taarifa iliyo sahihi; au

(b) itawataarifu wanachama na Mkurugenzi kuhusu makosa au upotovu.

Uchunguzi wa Mkurugenzi.

**57.**-(1) Mkurugenzi anaweza, kwa maamuzi yake, au atalazimika kwa maelekezo ya Waziri, kama itakavyokuwa, au kwa maombi ya wajumbe wasiyopungua theluthi moja ambao walikuwepo na kupiga kura katika mkutano wa Chama cha Ushirika ambao ulitangazwa vya kutosha, kufanya uchunguzi au kumtaka mtu yeyote aliyemuidhinisha kwa maandishi kufanya uchunguzi katika Sheria ndogo, hali ya utendaji kazi na kifedha ya Chama chochote cha Ushirika.

(2) Maofisa na wanachama wa Chama cha Ushirika watatoa fedha taslimu, hesabu, vitabu, nyaraka na dhamana za Chama cha Ushirika, na watatoa taarifa kuhusiana na shughuli za Chama cha Ushirika, iwapo mtu anayechunguza anaweza kuhitaji.

(3) Mkurugenzi atatoa taarifa ya matokeo ya uchunguzi katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Ushirika na atatoa maelekezo ya utekelezaji kwa mapendekezo ya ripoti ya uchunguzi.

(4) Endapo Mkurugenzi ataridhika, baada ya uchunguzi wa kina, kwamba Kamati ya Uongozi au Kamati yoyote ya Chama cha Ushirika haikutekeleza majukumu yake vizuri, anaweza:

(a) kuivunja Kamati; na

(b) kuwezesha kuteuliwa Kamati ya muda itakayoundwa na wajumbe wasiozidi watano miongoni mwa Wanachama wa Chama cha Ushirika kwa kipindi kisichozidi siku tisini.

(5) Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, atakuwa ni mkosa na atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili za Kitanzania kwa kila siku kosa hilo litakapokuwa linaendelea.

Ukaguzi wa kawaida wa vitabu vya Chama cha Ushirika kinachodaiwa.

**58.** Mkurugenzi anaweza, katika mazingira na namna inavyoelezwa katika Kanuni, na kwa maombi ya mdai wa Chama cha Ushirika, kufanya ukaguzi wa kawaida au kuwataka baadhi ya watu kwa maandishi kufanya ukaguzi wa vitabu vya Chama cha Ushirika.

Gharama za uchunguzi na ukaguzi wa kawaida.

**59.**-(1) Endapo uchunguzi utafanywa chini ya kifungu cha 57 (1) cha Sheria hii, au ukaguzi wa kawaida utafanywa chini ya kifungu cha 58 cha Sheria hii, Mkurugenzi anaweza, kwa hati atakayoitoa, kutoa amri ya kutenga gharama, au sehemu ya gharama hizo akiona inafaa, baina ya Chama cha Ushirika, wanachama au mdai anayetaka kufanyiwa uchunguzi au ukaguzi wa kawaida, na maofisa au maofisa waliotangulia wa Chama cha Ushirika; na maamuzi ya Mkurugenzi kwa mukhtadha huo yatakuwa ni ya mwisho.

(2) Kiwango cha fedha kilichotolewa kwa njia ya gharama chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitakuwa ni deni la madai litakalolipwa papo hapo kwa kutolewa hati iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Ukaguzi wa kushtukiza.

**60.** Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 58 cha Sheria hii, Mkurugenzi anaweza, kila baada ya muda, kufanya ukaguzi wa kushtukiza juu ya mambo ya fedha, sheria ndogo na shughuli za Chama cha Ushirika.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO

Muhuri rasmi.

**61.** Mkurugenzi atakuwa na muhuri rasmi utakaowekwa katika hati ya usajili iliyotolewa kwa Chama cha Ushirika na nyaraka nyengine zilizotolewa na Mkurugenzi kwa masharti ya Sheria hii.

Kuwasilisha ripoti ya mwaka.

**62.**-(1) Chama cha Ushirika kitawasilisha kwa Mkurugenzi ripoti ya mwaka.

(2) Ripoti ya Mwaka iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itakuwa na taarifa kama zilizoainishwa katika Kanuni.

(3) Chama cha Ushirika ambacho kimekiuka masharti ya kifungu hiki, kimetenda kosa na kitawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano za Kitanzania.

Uwezo wa kutunga Sheria ndogo na maudhui yake.

**63.**-(1) Chama cha Ushirika kilichosajiliwa kitakuwa na uwezo wa kutunga Sheria ndogo kwa utaratibu na maeneo ya Sheria ndogo hiyo kama itakavyoelezwa na Kanuni.

(2) Chama cha Ushirika kilichosajiliwa kitakuwa na uwezo wa kurekebisha Sheria yake ndogo kupitia azimio maalum la Mkutano Mkuu.

Kosa linalohusiana na usajili au leseni.

**64.** Chama cha Ushirika ambacho kinaendesha shughuli zake bila ya usajili au leseni halali, kama itakavyokuwa, kimetenda kosa na kitawajibika kulipa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano za Kitanzania.

Makosa ya jumla na adhabu.

**65.** Chama cha Ushirika au Mwanachama wa Chama cha Ushirika ambaye ametenda kosa lolote au amekiuka masharti ya Sheria hii ambapo adhabu yake maalumu haikutajwa chini ya sehemu yoyote ya Sheria hii, atawajibika kulipa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano za Kitanzania.

Ada.

**66.** Chama cha Ushirika kitalipa ada kuhusiana na mambo yafuatayo:

(a) kufanya usajili;

(b) ukaguzi wa hesabu, uchunguzi na ukaguzi wa kawaida wa hesabu za Chama cha Ushirika kwa maombi ya wanachama au wadai;

(c) tozo kuhusiana na makosa yaliyotendwa na Chama cha Ushirika kilichosajiliwa au mtu yeyote; na

(d) jambo jengine lolote ambalo kwa jambo hilo inatozwa chini ya masharti ya Sheria hii.

Waziri anaweza kufanya mapitio ya faini na ada.

**67.** Waziri anaweza kila baada ya muda kufanya mapitio ya faini na ada zilizoelezwa chini ya Sheria hii.

Uwezo wa Waziri kutunga Kanuni.

**68.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa utelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga Kanuni mahsusi kuhusiana na:

(a) taratibu za usajili;

(b) idadi ya juu ya hisa au sehemu ya mtaji wa Chama cha Ushirika anayoweza kumiliki mwanachama;

(c) fomu zitakazotumika na masharti yanayoambatana katika kufanya maombi ya usajili ya Chama cha Ushirika na taratibu zinazohusiana na mambo ya maombi;

(d) kuhusiana na mambo ambayo Chama cha Ushirika kinaweza kuyatungia sheria ndogo na taratibu za kufuatwa katika kuziandaa, kubadilisha, na kurekebisha sheria ndogo;

(e) masharti ya kufuatwa na mtu anayeomba kukubaliwa uwanachama na masharti yanayoelezea uchaguzi na kukubalika wanachama na malipo yanayohitajika kufanywa na maslahi yatakayopatikana kabla ya kuwa na haki ya uwanachama na masharti yanayoelezea ukomo wa uwanachama;

(f) namna fedha zinavyoweza kuchangishwa kwa njia ya hisa, rehani au vyenginevyo na namna ya maombi ya msaada wa kifedha kutoka Serikalini na benki yoyote au taasisi yoyote ya fedha yatakavyofanywa;

(g) masharti ya Mkutano Mkuu wa wanachama na utaratibu wa mkutano huo;

(h) masharti ya uteuzi na masharti ya uwajiri wa wafanyakazi wa Chama cha Ushirika;

(i) masharti ya uwasilishaji ya makadirio ya mwaka kwa ajili ya kupata ridhaa ya Mkurugenzi;

(j) uchapishaji wa mizania ya kila kipindi inayoonyesha mali na dhima ya Chama cha Ushirika;

(k) masharti yanayoelezea watu ambao kwa namna ambayo nakala za taarifa zinazoweza kuingizwa katika Vyama vya Ushirika zitathibitishwa;

(l) namna litakavyokuwa daftari la wanachama na taarifa zinazopaswa kuingizwa katika daftari hilo;

(m) aina ya Chama cha Ushirika kitakachosajiliwa; na

(n) muundo wa malipo ya huduma zitakazotolewa kwa Chama cha Ushirika.

Kufuta na kubakiza.

**69.**-(1) Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya mwaka 1986 inafutwa.

(2) Kifungu cha 2(1)(d) cha Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Nam. 12 ya mwaka 2012 kinafutwa.

(3) Bila ya kujali ufutaji chini ya kifungu kidogo cha (1) na kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki jambo lolote lililofanywa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litachukuliwa kwamba limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar tarehe 3 Disemba, 2018.

..................................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.***